



TAARIFA ZA HARAKA KUHUSU

Mabadiliko Yanakuja kwa Wasajiliwa wa Medicaid, Child Health Plus, na Essential Plan

NY State of Health ni Soko Rasmi la Mpango wa Afya la New York.

Ikiwa una miaka 19 au zaidi na unaishi katika Jimbo la New York, tunaweza kukusaidia kupata bima ya afya unayoweza kumudu.

Je, nitajisajili vipi?

📍 nystateofhealth.ny.gov

AU

📞 1-855-355-5777 au
TTY: 1-800-662-1220

AU

📄 Kupitia usaidizi uliobinafsishwa wa bila malipo kutoka kwa msaidizi aliyeidhinishwa karibu na nyumbani au kazini kwako.

NY State of Health inafuata sheria za haki za raia za Taifa na sheria za jimbo zinazotumika, na haibagui kwa msingi wa mbari, rangi, jinsia, umri, asili ya kitaifa, imani/dini, hali ya ndoa/familia, rekodi ya kukamatwa, hatia ya(z)ajina, utambulisho wa jinsia, mwelekeo wa kingono, sifa za kinasaba, hali ya jeshi, hali ya mwathiriwa wa unyanyasaji wa nyumbani, na/au kulipiza kisasi.

Je, wewe au mwanafamilia kwa sasa ana bima ya afya kwa New York State Medicaid, Child Health Plus au Essential Plan?

Jimbo la New York hivi karibuni litaanzisha upya ukaguzi wa ustahiki ili kuhakikisha kwamba wasajiliwa bado wanastahili kwa mipango hii. Hii imaanisha unaweza kuhitaji kuchukua hatua ili kuandikisha upya bima yako ya afya au bima ya wanafamilia wako. Kwa mfano, ikiwa mapato yako yamebadilika sana kuanzia kabla ya janga la COVID-19 kuanza, inawezekana kwamba unaweza kuhitaji kuripoti taarifa hiyo kwa NY State of Health ili kuendelea kusajiliwa katika bima ya afya.

Hapa ni baadhi ya mambo unayoweza kufanya sasa ili kujiandaa:

1 Jisajili kwa taarifa za ujumbe wa maandishi.

Jisajili kupokea taarifa za Ujumbe wa SMS/MMS kutoka kwa NY State of Health ili usikose taarifa muhimu kuhusu bima ya afya, ikiwa ni pamoja na wakati wa kuandikisha upya bima yako. Ili kujisajili, **tuma ujumbe unaosema START kwa 1-866-988-0327.**

2 Hakikisha kwamba anwani yako imesasishwa.

Hakikisha kwamba NY State of Health au ofisi ya Medicaid ya eneo lako ina anwani yako ya sasa ya barua, nambari ya simu na anwani ya barua pepe ili waweze kuwasiliana nawe kuhusu bima yako ya afya.

Ikiwa una bima katika NY State of Health, unaweza:

- Kupiga simu kupitia 1-855-355-5777 (TTY: 1-800-662-1220)
- Kuingia kwenye akaunti yako katika nystateofhealth.ny.gov
- Kupata msaidizi katika <https://info.nystateofhealth.ny.gov/findassistor>

Ikiwa una Medicaid kupitia kwa ofisi ya Medicaid ya kaunti yako au kupitia New York City's Human Resources Administration (HRA), wasiliana na ofisi ya eneo lako utoe anwani yako na maelezo yako ya mawasiliano.

3 Fuatilia habari mpya.

Tembelea <https://info.nystateofhealth.ny.gov/COVID-19-Changes> ili kujifunza zaidi. NY State of Health itasasisha ukurasa huu mara kwa mara kwa taarifa mpya.